**Translator:** His name is Sironga.

**Ole Ndiambut:** *Ole ngae*

**Translator:** Sironga ole Tekka.

**Com. Githu Muigai:** Okay, point yako tumeichukua, any other point?

**Speaker:** Zko nyingi.

**Translator:** We can give to the Commissioners they know how to read. *Etejo eikisum iyiook ena toki badala naisumakini iyiook*

**Com. Githu Muigai:** Okay, hii memorandum tumeshika mzee na tumeshukuru sana Bwana Sironga asante sana. Wazee tusonge mbele hivi, tunaleta watu hapa sasa tutafuatana hivi. Yule mtu hajazungumza akaribie hivi viti vya mbele, wote tuzungumza msiwe na haraka.

**Translator:** *Etejo entinyiku iltungana pooki leton eyieu neuro.*

**Com. Githu Muigai:** Ketini vizuri hapa mbele, wale watu hawajazungumza karibieni mbele. Kila mtu atazungumza.

**Speaker:** *Ore taa entoki ai e dukuya naa enashe tenkaraki ena olong.*

**Translator:** Anasema ya kwanza ni kushukuru kwa siku ya leo.

**Speaker:** *Ore ena olong naa enkolong sapuk oleng .*

**Translator:** Leo ni siku kubwa sana.

**Speaker:** *Nikincho enkai enashe amu ore ena naa enalotu aitayu inkeru o isiraeli temisiri.*

**Translator:** Hii Katiba ya leo ni kama ile ya kuondoa watu Misiri kupeleka Kaanan.

**Speaker:** *Naa kaliki kulo komishiona orikoo ena siaai ajoki ewaita ina siaai oleng.*

**Translator:** Anawaomba Commissioners mjaribu kuchukua hii kazi vilivyo.

**Speaker:** *Eminchoso entoki nikiro tenewueji nemitabayaya.*

**Translator:** Si tuje tukae hapa lakini hamtafikisha.

**Com. Githu Muigai:** Tutafikisha mwambie tutafikisha.

**Speaker:** *Amu ekisujita ekisujita ajo kainyoo opa kitejo natase etejo ekitabaya, ore taa engae toki e dukuya naa ene nkop nimiba nikijo amu enoki nainosita iyiook oleng.*

**Translator:** Anasema yake ya kwanza ni kuhusu ardhi.

**Speaker:** *Nemiba nikijo amu ketanyamalita iyiook oleng.*

**Translator:** Anasema hiyo ni shida ambayo tuko nayo sana.

**Speaker:** *Ore entoki e dukuya naa kitejo atejo nanu pee eishori iyiook majimbo.*

**Translator:** Yeye anaomba Federal Government.

**Speaker:** *Amu ore enapa Serikali o lashumpa natulusoyie o enanyaka asuju neitu esaidia ninche iyook.*

**Translator:** Anasema wakati wa ukoloni na wakati wa Serikali hii sasa.

**Speaker:** *Naa ekyieu Serikali nalotu aisaidia iyiook.*

**Translator:** Ili wakati huu pia tuweze kufaidika.

**Speaker:** *Nabaiki iyiook too ngangitie adol osina.*

**Translator:** Kwa vile tumekaa kwa muda mrefu na shida.

**Speaker:** *Ore tiatua kulo tungana le Kenya naa ketii ilojo ninche ekira iyiook inguesi.*

**Translator:** Anasema kwa wakati mwingine wanakaa kama wanyama.

**Speaker:** *Nemekira enguesi.*

**Translator:** Na sisi sio wanyama.

**Speaker:** *Neaku ina pee kiyieu Serikali e majimbo nalotu aitore iyiook.*

**Translator:** Na ndio tuko hapa kubadilisha.

**Com. Githu Muigai:** Mwambie hiyo mambo ya kutengeneza Jimbo ya Wamaasai inaitwa South Rift, tumeishika na kuiandika. Tusonge mbele.

**Translator:** *Etejo taa ore ina naa etejoki naji keji south rift neaku ore esiaai e jimbo eidipe nai.*

**Speaker:** *Ore sii enkae ore ene jimbo naa enosotua*

**Translator:** Anasema kuhusu hiyo Jimbo ni kuhusu amani.

**Speaker:** *Entoki napiki sheria osotua.*

**Translator:** Ni kitu cha kutuletea amani.

**Com. Githu Muigai:** Tumekubali hata sisi, tuende kwa point nyingine.

**Speaker:** *Enkisuma sii .*

**Translator:** Itaweza kutuletea elimu karibu.

**Speaker:** *Naa ekyieu nikisum inkera ebaiki enkilasi nabo omitabaikini university.*

**Translator:** Anasema itawezesha labda hata kuelimisha watoto kutoka darasa la kwanza mpaka university.

**Speaker:** *Amu ore pee kijeito kajeito nijiaa ara ilmaasani kadolta ajo ekiata oshi impisai ang.*

**Translator:** Anasimama hapa akisema kuwa labda kuna haki ya Maasai ama pesa zao.

**Speaker:** *Kidolta ajo ore oshi anaa magadi soda.*

**Translator:** Anasema kuhusu kampuni ya Magadi Soda.

**Speaker:** *Anaa nationl bak*

**Translator:** Ans National Park.

**Speaker:** *Oltukai.*

**Translator:** Oltukai.

**Speaker:** *sambur lorge*

**Translator:** Samburu Lodge.

**Speaker:** *Maasai mara.*

**Translator:** Maasai mara.

**Speaker:** *enaiposha.*

**Translator:** Naivasha

**Speaker:** *Naa keitsheiki haki inkera o maasai neitasheiki kulie e Kenya. amu haki ang naa.*

**Translator:** Anasema kodi ya hizo ma kampuni zote ametaja zinaweza kuelimisha watoto wa Maasai.

**Com. Githu Muigai:** Okay.

**Speaker:** *Neaku ekigira ajo pee ereti iyiook te nkisuma oleng.*

**Translator:** Bado tunaomba elimu tusaidiwe iwe ya bure.

**Speaker:** *Ore tenakata iyiook neton etii emodai oleng .*

**Translator:** Saa hii ni vile sisi hatujaelimika ndio tuko wajinga.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo mzee tunakubaliana na wewe, tumeandika tayari, tumeambiwa kutoka asubuhi, elimu kutoka class ya kwanza mpaka ya nane iwe bure, hiyo tumeandika. Kwa hivyo tusonge mbele ndio kila mtu apate kuzungumza.

**Translator:** *Etejo taa ore pee etum pooki ngae airoro ore ntokitin duo naimakaki keigero pooki neaku meeta haja pee intoki aingil neaku ore pee iyata entoki ngejuk ingila.*

**Speaker:** *Ore sii enkae toki naidim ainyiaki atolimu.*

**Translator:** Anasema ile atasema haijaguzwa.

**Speaker:** *Naa esiaai o ntomonok.*

**Translator:** Ni kuhusu wanawake.

**Speaker:** *Pee etum sii ninche intasati oo ilmaasai erikore.*

**Translator:** Hata uongozi unahitajika hata akina mama Wamaasai wapate uongozi.

**Speaker ;***Kake ata tenaa president eyieu naa peaku tiabori olpayian etii.*

**Translator:** Anasema kuwa hata kama mama wa Kimaasai watapata uongozi.

**Com. Githu Muigai:** Wapewe vitu vya uongozi.

**Speaker:** *Naishu nanu teine.*

**Translator:** Anasema anamalizia hapo.

**Com. Githu Muigai:** Haya tumefurahi sana, umetoa maneno mazuri sana mzee asante, jiandikishe hapo. Next.

**Speaker:** *ayieu kalimani.*

**Com. Githu Muigai:** Unaanza mzee tafadhali kwa kutupatia jina lote ndio tuweke kwa tape. Sema jina lako ni nani?

**Paul ole Kajira:** *Kaji Paul ole kajira*

**Translator:** Amesema anaitwa Paul ole Kajira.

**Paul ole Kajira:** Hata majina nimeandikisha huko *Etejo*

**Translator:** Anasema ataongea Kimaasai na jina lishaandikishwa huko.

**Paul ole Kajira:** *Aisho intai ilpayiani kulo le komishion tenkaraki engiriata inyi osotua linyi tenkaraki nidima ayetu ningiriri angamaa erorei pooki aisho intai enashe sapuk oleng.*

**Translator:** Anasema anarudishia commission hii shukrani kwa kuja kupokea maoni yote.

**Paul ole Kajira:** *Eiroroki inkumok naiusu duo iduaat ainei.*

**Translator:** Amesema mengi ambayo yamehusu maoni yake yamezungumziwa.

**Paul ole Kajira:** *Kaimaa ake nabo.*

**Translator:** Amesema ana moja tu.

**Paul ole Kajira:** Naunga mkono Majimbo, naunga mkono hii sheria ya *Pee etayuni sheria e enterit namba mia tatu naiumisa iyiook ilmaasai.*

**Translator:** Amesema anaunga mkono Serikali ya Majimbo, na pia kuunga mkono ile sheria ya mia tatu kumi na mbili ambayo imenyanyasa Wamaasai kuhusu ardhi.

**Paul ole Kajira:** *Aa ta entoki nabo naaku namba uni too duaat ainei.*

**Translator:** Anasema ana jambo ambalo ataongeza.

**Paul ole Kajira:** *Naa kajo eetai sheria apa natipika ilashumpa pee eya enkop o ilmaasai apuo aramatishore nejo ore pee kukondesha kwa arthi nejo etipika ilarin ntomoni naudo.*

**Translator:** Anasema kuhusu lease ya mashamba ambayo inachukua miaka tisaini na tisa, ambapo ardhi ya Wamaasai ilichukuliwa na Wazungu na labda ikiisha bado hatujajua namna vile inavyoendelea.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumeelewa.

**Paul ole Kajira:** *Ore ina sheria o ilarin intomoni naudo nemekure eidimayu amu meeta oltungani lenkata ilarin intomoni naudo.*

**Translator:** Anasema hiyo sheria sisi hatukubali ya miaka tisaini na tisa kwa sababu hatukuweco kwa hivyo tunataka ifanyiwe labda marekebisho.

**Paul ole Kajira:** *Meekure ebaya oltungani le taata ilarin ntomoni naudo teneini mebaya.*

**Translator:** Anasema hata ikitajwa hiyo miaka haiwezi fika.

**Paul ole Kajira:** *Neaku kigil ina kabisa amu ilashumpa apa otipka pee etum atotonie enterit o ilmaasai ina natii taata olosho lang lenaalo e naiposha.*

**Translator:** Anasema hiyo sheria ya hiyo miaka tisaini na tisa ifutiliwe mbali na ardhi irudishiwe wenyewe.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumekubali, hiyo tumesikia mzee tusonge kwa neno ambalo bado hatujasikia.

**Paul ole Kajira:** *Enikodeshai enterit amu ebaiki netii oltungani oyieu neikodesha aipedekeza nchere maishoo metaa ilarin tomon o imiet te nebik oleng mpaka tomon.*

**Translator:** Anasema labda kwa lease ya mashamba ipunguzwe badala ya miaka tisaini na tisa iwe labda inaenda miaka tano ikienda zaidi miaka kumi.



**Paul ole Kajira:** *Atejo ilarin tomon omiet mpaka tomon.*

**Translator:** Kumi na tano hadi kumi.

**Paul ole Kajira:** *Basi naisho intai enashe*

**Translator:** Anasema anashukuru.

**Paul ole Kajira:** *Enikitum majimbo ore kuna kulie pooki neleleku.*

**Translator:** Anasema tukipata Majimbo itakuwa ni sawa.

**Paul ole Kajira:** *Ashe oleng.*

**Com. Githu Muigai:** Asante sana mzee. Keti hapa mzee, uko next baada ya huyu mwenye tie. Madam it is you next do not worry, we need to get through this na sasa tukimaliza akina mama watakuja mbele. Yule mtu ambaye hajazungumza na anataka kuzungumza akaribie. Sasa mzee, fanya heshima sana hawa watu wote walikuja saa moja asubuhi na bado wako, tufanye heshima kwa kila mtu dakika mbili mbili na tusirudie mambo, tumesikia mambo mengi tusiyarudie. Lakini uweke tu ile nguvu na mkazo. Asante.

**Laparmwat:** *Airoroki intai pooki te nkarna e yesu entasupa pooki.*

**Translator:** Anawasalimu wote, hamjambo?

**Com. Githu Muigai:** Upatiane jina tafadhali mzee nilisahau kukuambia.

**Laparmwat:** *Kaji tinga ole parmuaat.*

**Translator:** Anaitwa Laparmwat.

**Laparmwat:** *Naa oltepesi ainguaa sub location.*

**Translator:** Na anatoka Oldepesi Sub Location.

**Laparmwat:** *Cenrtral keek onyokie.*

**Translator:** Central Kiokonyokia.

**Laparmwat:** *Aidoropu najo oleng amu eiroroki inkumok eiroroki inkumok eiroroki ninye duo nayieu najo eiroroki pooki.*

**Translator:** Anasema karibu yote yale angezungumzia yamezungumziwa.

**Laparmwat:** *Naa kanyor airoro intokitin are ake*

**Translator:** Na atataja mambo mawili tu.

**Laparmwat:** *Ore ene dukuya enaa enairoroki naa majimbo naa kaiunga mkono ina Serikali e majimbo.*

**Translator:** Anasema yeye anazungumza kuhusu Serikali ya Majimbo, anaiunga mkono kwa dhati.

**Laparmwat:** *Tenkaraki kadol ajo ore ninye kira iyiook Kajiado north .*

**Translator:** Kama sisi wananchi wa Kajiado North.

**Laparmwat:** *Mikiata ata college o ilmalimuni*

**Translator:** Hatuna mambo mengi hata mashule hayana waalimu.

**Laparmwat:** *aata iloo ldakitarini.*

**Translator:** Hata kuhusu madaktari.

**Laparmwat:** *Naa ekidol ajo tenikitum nayo majimbo*

**Translator:** Tukisema Majimbo.

**Laparmwat:** *Naa keponu naa aanyikaki iyiook lelo matuda pooki matodol sii iyiook tena nkop.*

**Translator:** Na kama yale hatukuwa nazo kama waalimu ama madaktari tutapata hayo matunda.

**Laparmwat:** *Ore entoki kiata museum tede.*

**Translator:** Na anasema hapo karibu na kwao kuna pre-historic site.

**Laparmwat:** *Ore in museum.*

**Translator:** Hiyo museum iko hapo.

**Laparmwat:** *Naa atua inkshi ang etii.*

**Translator:** Iko kwetu.

**Laparmwat:** *Nitu aikata iyiook kidol olganayioi ata obo likinosa.*

**Translator:** Hatujawahi kupata chochote kutokana na hiyo museum.

**Laparmwat:** *Nija etiu esiaai e makat oo nemakaki duo magadi soda.*

**Translator:** Na kuhusu Magadi, wengine wametaja.

**Laparmwat:** *Nekiyieu duo naai ore itokitin nijo nena naa kekiramatishore niktum sii iyiook faida tenkaraki aa enkop ang etii.*

**Translator:** Anasema hizo natural resources zote ziko lazima tupata faida kutokana nazo.

**Laparmwat:** *Eimakaki duo esiaai o nguesi .*

**Translator:** Na hali ya wanyama wa mwiti.

**Laparmwat:** *Ore ena ina kesipa pii kesipa, kesipa tenenya taata enkiteng olowuaru ashu oltungani pee iar iyie ilo owuaru ashu iar enkolii nikimbungi iyie nemikinchori iropiyani ina kiteng ino amu einosita engues.*

**Translator:** Anasema kuhusu wanyama wa mwitu labda wakati mwingine wanaua mifugo wetu, wanaua watu wetu, lakini sisi tukiwauwa tunakamawa lakini hao wakifanya hiyo ..

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumesikia kutoka asubuhi mzee na tumekubaliana.

**Laparmwat:** *Ore amu itoningo aomon intai etabai te nkarna enkai nena kirorot anaa enikitejo tenewuei ashe oleng.*

**Translator:** Anasema kwa vile mmesikia ni ombi lake kutia mkazo mfikishe na iweze kutimika.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana. Yes.

**Peter ole Nchoki:** Honourable Commissioners sitarudia yale yamesemwa, nitajaribu kusema ..

**Com. Githu Muigai:** ....(Inaudible) Endelea. Taja majina kwanza.

**Peter ole Nchoki:** Nataka kutoa habari ya symbols of business, yaani kutumia alama ya kabila fulani kufanyia bishara.

**Com. Githu Muigai:** Unajua tuna-record kila kitu ndio tujue moni ni yako lazima uanze na jina lako, useme mimi naitwa fulani.

**Peter ole Nchoki:** Mimi naitwa Peter ole Nchoki.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana Peter, endelea.

**Translator:** *Etejo taa keji Peter ole Nchoki.*

**Peter ole Nchoki:** Na nimeenda sehumu nyingi sana na mimi naona, nakuta alama ya Maasai, tourism Maasai na sijaona kabila lingine.

**Translator:** *Etejo ashomo taa inkuapi kumok nadol imbaa.*

**Peter ole Nchoki:** Hao watu wamepata pesa nyingi kwa kutumia pesa nyingi kwa kutumia jina la kabila fulani.

**Translator:** *Nejo sii ore lelo tungana enotito impisai kumok.*

**Peter ole Nchoki:** Sasa maoni yangu ni kwamba mtu yeyote katika sheria mpya ambaye atapatikana akitumia alama ama jina la kabila fulani kufanya biashara hukumiwe kisheria.

**Com. Githu Muigai:** Basi, hiyo tumeandika.

**Peter ole Nchoki:** Ya pili ni mambo ya umaskini/ poverty. Tukitaka kumaliza sheria moja uangalie sana mambo ya ukulima – agriculture, itiliwe mkazo. Maoni yangu ni kwamba Commission ya watu katika jamii fulani iteuliwe isimamie Ministry officials kutoka district levels wawe wakiangalia mambo ya ukulima wahakikishe kwamba mtu wamelima, na watu watafanya bidii na njaa itapotea, na umaskini tutamaliza. Yaani commission ichaguliwe.

**Com. Githu Muigai:** Asante hiyo tumeshika.

**Peter ole Nchoki:** Nataka kuguzia mambo ya inheritance ya wasichana. Inheritance ya wasichana ni kweli kwa sababu mila yetu hairuhusu wasichana warithi mali ya mzazi lakini ningetaka kusema iruhusu lakini wale wasichana ambao hawajaolewa. Kama msichana hajapata bwana apatiwe urithi kwa wazazi. Mimi naonelea hiyo ni muhimu lakini yule amepata bwana arithi kwa bwana yake.

Mambo ya elimu nitaongeza kitu mpya, pastoralists wanakuwa na shida ya kuhama hama, sheria mpya ikibuniwa. Serikali iangalie kama kutakuwa na boarding primary school katika every location of the pastoralists' districts ndio wakihama tena wakati wa kiangazi watoto wasihame kufuata ngombe. Hiyo sasa ninapendekeza pastoralists primary boarding schools. Ni hayo tu waheshimiwa.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana tusonge mbele, tuendeni hivi mama kwanza halafu... na huyu mzee amerukwa na watu wengine sana, sasa lakini ni gentleman kwa hivyo atakubali akina mama kwanza halafu yeye. One minute, kwanza mzee kwa sababu amesimama halafu ... okay, mzee sasa ni wewe anza na jina halafu nitaombea ruhusu mwenye kutafsiri ile gari anaenda nayo karibu itaondoka tafadhali tumpatie dakika mbili amefanya kazi mzuri mzee akimaliza tuende kwake halafu akina mama.

**Zakary Mwangi:** Asante sana bwana mwenyekiti na Commissioners wote, mimi nitajaribu sana kuwacha kuongea juu ya kitu ambacho kimetajwa lakini labda nitaenda on new grounds.

**Com. Githu Muigai:** Umeanza na jina, tafadhali?

**Zakari Mwangi:** Jina langu ni Zakary Mwangi a registered voter, Kajiado North constituency.

**Com. Githu Muigai:** Okay, endelea Bwana Mwangi.

**Zakari Mwangi:** The type of Government that we would require, I recommend that we have a Unitary Government in Kenya with an executive President and a Vice President.

Election, I would say and I recommend that any candidate vying for Presidency should be above 45 years of age. Asante sana, kwa hivyo mimi nasema kwa habari ya uchaguzi, upande wa Rais, yule candidate ambaye atasimama awe at least 45 years of age na tena akiwa declared yaani atangazwe ati ameshinda awe amepata at least 51% of the total votes ya Kenya na katika 6 provinces awe ame-win, outright win kwa six administrative provinces as at now, zile ziko, hatujihi kama zitakuwa nyingine.

Parliamentary election, mimi nina-recommend at least 35 years kwa Parliamentary candidate na tena akiwa-declared ati ndiye...*(Incomplete)* votes ya hiyo constituency na tena kama hiyo constituency wale registered voters hawatatimiza 33% voters wale registered wale watakao-vote kama hawatimiza 33% ya registered votes, hiyo place iwe-declared wame-boycott wakae miaka tano bila MP ama bila Councillor. Kwa hivyo naye mwenyewe awe-sponsored by a political party hatutaki independent candidate, awe amekuwa supported, nominated whatever criteria ile party itatumia hiyo ni yao si yetu.

Haya tukiingia katika political parties niki-recommend political party yoyote ambayo haina mjumbe Parliament wasikubaliwe kusimamisha a Presidential candidate kwa sababu atasimamia nini. Tena all political parties after elections those who are registered, political party yoyote ambayo haitapata at least wabunge watano, hatutaki lone rangers, 5 Parliamentary candidates waingie Parliament, they dissolve themselves peacefully and quietly, wale wamechaguliwa waingie parties of their own choice. Hatutaki one Parliamentary candidate wengine hawana mtu katika Parliament, wengine hawana wajumbe. I recommend that we discontinue that.

**Com. Githu Muigai:** Umebakisha dakika mbili.

**Zakary Mwangi:** Pole sana Chairman, can I go ahead please? Thank you.

During and after elections kuna mambo hiyo yote ni ya usalama na ya rigging, let the right arms of the Government take care of that, na Electoral Commission ipewe nguvu sana ya ku-prosecute those election errors.

Ile nyingine ni kuhusu period ya elections, Kenya mpaka leo utakubaliana na mimi hatujui election ni ya lini, iwe at a fixed date after 5 years kama US. Tunajua US elections is on the first week of November hiyo inajulikana through out the world. Isiwe ati mara hii au mara hii, kwa hivyo iwe at a fixed date.

Katika upande wa by-election, by elections imetuumiza sana iwe lazima 33% wawe ndio wana-vote.

On freedom, hii labda iko katika current Constitution, freedoms tofauti lakini ile nataka zaidi kutaja ni freedom of worship. Nataka hiyo kwanza iwekewe mahanani labda ni mapenzi yenu Commissioners iwekewe maanani. Ningependekeza all our security arms ambao wanalinda usalama wasiingie katika Parishes ama Mosques kufukuza waumini kama ilivyofanyika All Saints Cathedral, let us not have such a thing again in Kenya.

**Com. Githu Muigai:** Tuendeleo, tumechukua hiyo.

**Zakary Mwangi:** Asante. Yaani wasiingie, na ninauliza all Clergy men, the Imams ama the Christians wapewe ile tunasema immunity, they cannot be arrested when they are inside their compounds katika Kanisa wawe na immunity kama diplomats.

On Police Cells, hebu tusifanye Police cells zetu kama jela zingine yaani pre-determined detention yaani you are guilty before you prove yourself, tondoe hiyo katika Katiba yetu. Na tukiingia katika Law Courts ile backlog ambayo iko ma-cases mengi sana, I have got this recommendation ati case kama ni yangu ama yako ama ya mwingine kama imekwisha leo submissions ya defence today, judgement iwe on the same day.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumeshika.

**Zakary Mwangi:** Ikiwa inaairishwa ati ni wakati mwingine, chances of influencing the Margistrate are very rive, nitaenda huko nimhonge.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumesikia, justice should be prompt. Tuende point yako ya mwisho tafadhali.

**Zakary Mwangi:** Justice iwe prompt.

Haya on our own prisons, labda kila mtu anafahama lakini ile zaidi na-recommend katika prisons ni kutokana na ile sheria ilianza kutumika sometimes back sijui mwaka huu ama mwaka uliopita. Canning was abolished in schools na hao ni watu below 18, how do you cane an adult? Canning iwe abolished in our prisons.

**Com. Githu Muigai:** Very good point.

**Zakary Mwangi:** Canning be substituted with hard labour, ku-cane mzee ni aibu.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumesikia mzee, asante sana, actually one of his better points.

**Zakary Mwangi:** Ile nyingine is on economy, nikienda kidogo economy yetu hata ikiwa si mzuri ama ni mbaya that is not your concern, kwa sababu wakati mfuko yako haina kitu economy ni mbaya ikiwa na kitu economy ni mzuri.

Dream; tulisema during independence and after independence in the year 2000 there will be piped water in every home, today even the water is not there leave alone the piped water, the water is not there. Today we are crying of industrialization when we are killing our industries. Tuanzishe industries like Jua Kali na tuzipe all the necessary materials za kuweza kuendeleza biashara.

Development priorities, sisi hatuna priorities in Kenya.

**Com. Githu Muigai:** Tatadhali tusikize, tafadhali hapo wazee, ngojeni kidogo tu dakika moja.

**Zakary Mwangi:** Sisi hatuna priorities in Kenya yaani tunasema hivi, tommorow it is there, the next day unasikia iko there na hii ni kwa sababu kamati zile ambazo ni za district DDC are toothless bulldogs.

**Com. Githu Muigai:** Pendekeza tafadhali.

**Zakary Mwangi:** Napendekeza iwe lolote litakuwa recommended at the locational level to the divisional level ati wanataka any development project up to the district iwe taken seriously by the Central Government bila kugeuzwa ati ni hivi ama ni hivi, we do not want that.

**Com. Githu Muigai:** Nitakuuliza ukomeshe hapo tafadhali kwa sababu bado tuna watu wengi, umesema mambo mengi mazuri na uko na memorandum tutasoma hayo mengine. Kuna swali moja tu.

**Com. Wambua:** Mwangi.

**Zakary Mwangi:** Chairman with your permission nitaje moja tu.

Ninge-recommend habari ya Ministers, I take off my hat to one of the Ministers ulisema tusitaje majina na hatutaki. Just last Sunday alisema Government ya Kenya inakuwa let down by the inability of some Cabinet colleagues ambao hawawezi ku-interpret the policies, alisema ukweli ninamtolea kofia hiyo kwa sababu kuna wengine ambao hawajui ku-interpret na kwa

hivyo ukiwa Minister...

**Com. Githu Muigai:** Unapendekeza nini?

**Zakary Mwangi:** Napendekeza ukiwa Minister lets say, Defence or Internal Security et.c uwe na at least qualification zinazohusiana.

**Com. Githu Muigai:** Za kutosha, kusiwe wajinga ndani ya Serikali.

**Zakary Mwangi:** That is okay.

**Com. Githu Muigai:** Basi hiyo tumeelewa, basi tusonge mbele. There is a question for you.

**Com. Wambua:** Mzee Mwangi, nina swali kidogo. Ulipotaja mambo ya systems of Government vile ulikuwa unataka ukasema mambo ya President na mambo ya constituency elections iwe 33%, ulikuwa unasema hapo tunataka, plural halafu baadaye ukaanza hapo napendekeza. Ulipokuwa unasema tunataka ni wewe na nani, uko na group ulikuwa unawakilisha ama ni maoni yako ulichangia?

**Zakary Mwangi:** Mimi najiakilisha.

**Com. Githu Muigai:** Okay, asante Bwana Mwangi. Mkalimani wetu na uchukue dakika mbili gari lako lisikuwache.

**Daudi ole Lemondoi:** Sawa sawa nitachukua dakika mbili, kwa majina kwanza mimi ni Daudi ole Lemondoi kutoka Sonorua, ningependa kutoa maoni yangu kwani mengi nilikuwa nayo yamezungmzwa na sitachukua muda kurudia.

Kwanza kuhusu corruption, ningelipenda Katiba ipatie nafasi Anti-Corruption Authority nguvu ya kusaka maofisa wote wa Serikali ambao wanahusika na ufisadi.

Vile vile kuhusu elections ningependa kugusia mambo mawili, ningelipenda Chairman wa Electoral Commission asiwe anachaguliwa direct na President kwa sababu hata President ni mchezaji kwenye huo uwanja. Kwa hivyo anastahili labda amchague lakini awe amependekezwa na wabunge. Wawe wamepatia labda majina mawili ama matatu anachagua miongoni mwao, Chairman wa Electoral Commission, ama Tume ikichaguliwa, Tume yenyewe ichague mwenyekiti wao.

Lingine ni kuhusu nomination ya MPs and Councillors, tunaona labda wakati mwingine wananchi wanakataa Councillor ama Mbunge kisha anateuliwa anaenda Bunge ama Council na anakuwa Waziri. Kwa hivyo tunaona heri yule ambaye amesimama



na akashindwa kwa kura na wananchi asipewe nafasi kuwa nominated achaguliwe yule hayuko nominated.

Jambo lingine, tunaona kuwa tuna wazee manyumbani wanafika umri fulana hata wanakuwa hawajui vile wanasema ama vile wanafanya, hata Rais, tupendekeze Rais wa nchi yetu umri wa mwisho, mimi ningelipendekeza aanzishe akiwa na miaka 35, a-retire akiwa na miaka 65. Yule atapita hapo asikuwe Rais wa jamhuri ya nchi hii.

Vile vile kuhusu elimu, kuna jambo moja liliwachwa nje na ndivyo tuko hapa siku ya leo tungemaliza wakati mlikuwa siku ya kwanza. Hakusomeshwi elimu ya uma ama civic education kwenye mashule na ndivyo siku ya leo tumerudi hapa tungemaliza last time kwa kuwa wengi wetu hawajui chochote kuhusu civic education, kuhusu Constitution, kuhusu chochote kile. Tungeliomba katika curriculum tupatie civic education nafasi ili labda wakati Katiba itabadilishwa tena na labda tutakuwa wazee ama tutakuwa tumekufa watoto wetu watakuwa wamesoma hayo mambo kwenye primary schools na kwa sababu kuna wengine wetu wamesoma mpaka form four na hawajui chochote kuhusu Katiba, heri iwekwe kwenye curriculum ndio wengine waanze kusoma.

Vile vile kuhusu public land, ziwe entrusted na community kuliko kuwachia County Council. Nadhani nitafikisha hapo, sina mengi. Asanteni sana.

**Com. Githu Muigai:** Asante tunakushukuru sana. Sasa ni akina mama tafadhali. Please start with your name for the record.

**Lilian Makuleiyo:** Thank you Commissioners, ladies and gentlemen. I am Lilian Makuleiyo from Kajiado. I will start with:

Parliament, it has no right to change the Constitution it should go to the people and get a consensus of 90%.

Women should be given 30% of Parliamentary and civic leadership.

Pastoralism should be introduced in the school curriculum.

Early pregnancy, I suggest that it be taken to ‘Olosho’ and I suggest that it be extended nationwide because I think it is a nationwide problem.

Did we talk about inheritance that a wife should inherit the husband’s property? Yes, I think that is all. Thank you.

**Com. Githu Muigai:** Thank you very much. Si wewe, wewe utaingia kwenye que inaenda hivi.

**Elizabeth Sialo:** Nawasalimu nyingi nyote katika jina la Yesu, nawasalimu mpaka Commissioners wote. Nimekuja hapa kwa ajili ya akina mama wale mabwana wao wamefariki, wanashida nyingi sana.

**Com. Githu Muigai:** Mama hilo jina ndio lingie kwa tape kwamba wewe ni fulani na ulizungmiza mambo fulani, anza kwa

“jina langu ni”... halafu tuendelee.

**Elizabeth Sialo:** Jina langu ni Elizabeth Sialo Munguti. Akina mama wale mabwana wao wamefariki wananyanyaswa sana kutokana na mali ile bibi amewachiwa na bwana yake. Kunyanyaswa ni kama vile labda bwana alikuwa ameo bibi siku moja ama mwezi moja na hakuzaa na yeye. Yule bibi anatoroka anaenda anaolewa pahali pengine, yule mzee anakaa na huyo bibi wanazaa wanne au watano mpaka hata mtoto wa kwanza anakuwa na watoto tano ama sita kama mtoto wa kwanza ameolewa. Yule mzee anaaga dunia, wakati ashaaga dunia baada ya miaka ishirini na nne hakuna complainant, na yule mama mwenye boma yule aliwachiwa na bwana amechukua ile mali kwa sababu watoto walikuwa labda wadogo akachukua ile mali akaandika kwa jina lake. Ikifika wakati wa kugawia watoto wake hiyo mali, wakati huo yule mama ambaye alienda bila mtoto anakuja na watoto kumi na sita anasema alikuwa ameolewa kwa hiyo boma.

**Com. Githu Muigai:** Pendekeza, ungependa sheria itengenezwe namna gani ndio mambo ya namna hiyo irekebishwe?

**Elizabeth Sialo:** Nataka Serikali itusaidie, Constitution itusaide kwa sababu tukienda kama wamepelekwa kortini inasemekana ati yule mama aliyekuja na watoto kumi na sita agawiwe mali na huyu mama mwingine ametaabika na watoto na bwana wake na alikiwa amemuwacha. Ni wengine sana wametaabika kutokana na hiyo shida sana.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumeshika, point nyingine?

**Elizabeth Sialo:** Sina nyingine.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana. Jiandikishe hapa, hiyo ni point ya maana sana.

**Victor Gatweku:** Thank you very much, my name is Victor Gatweku and I represent Ololoisei Welfare Association which is an association of various ethnic groups who are residents in Ngong. I must state right from the onset that I agree with those who have called for regional Government or devolving power to the regions yaani Majimbo. Hii si kwa Jimbo la Wamaasai peke yake bali iwe kwa Majimbo yote ya jamhuri ya Kenya, we devolve power to all regions. Kwa ufupi sana ningependa kutoa recommendations, when we devolve power to those regions, there are certain pertinent laws that must be put to safeguard the national stability and peace.

1. While regions would enjoy considerable autonomy, all citizens of Kenya would be free to live, to work, to school, to own property in any region and be accorded equal rights, privileges and protection.
2. Incitement to ethnic animosities should be classified as a treasonable offence with life imprisonment as its sentence, and anybody convicted of incitement should never hold a public office.
3. Any loss of life or property as a result of tribal or ethnic animosities should be compensated by the Government. We

have that as a very big problem in this country today, we know the issues of Molo, Enosopukia and all those other regions.

4. This autonomous regions will base their law, their rule and their regulations on the national Constitution so that we safeguard national stability and peace.
5. Finally when we devolve powers to those regions, tunapopatia watu uhuru wa Majimbo, Nairobi and Mombasa being economic centres should not be classified under any Jimbo, they should be under the control of the Central Government. Thank you.

**Com. Githu Muigai:** Thank you very much. Ngoja kidogo tu because you were very brief there is a questions for you, you did very well.

**Com. Wambua:** I did not quite understand and I want to follow it because I think it is a key issue. When you talk of devolution and you are saying that certain centres should belong to the central Government or to the nation which centres exactly are these, how do we define them?

**Victor Gatweku:** I have said Nairobi and Mombasa only because of their historical importance and the fact that they are the major economic centers, should not be classified under any Jimbo, they should come under the control of the central Government.

**Com. Wambua:** Asante sana.

**Com. Githu Muigai:** Thank you very much. Could we please try to emulate that example. Thank you very much, start with your name Sir.

**Joseph Wathigo:** My name is Joseph Wathigo Maanji. I am very grateful to get this opportunity and I will be talking because I want to contribute and I am likely to be a candidate for Kajiado North Parliamentary seat. First and foremost, I want to make an observation to the Commissioners, I came here very early in the morning at 7.00 a.m. and I registered as position 5 to speak but unfortunately we are speaking as the last people but we appreciate that. I will request an observation if may be tomorrow you come to this place or any other place it is also good you come with your people who will control the entrance and the list, it should be systematic to who is coming first. The criteria should be who comes first.

**Com. Githu Muigai:** Point well taken thank you.

**Joseph Wathigo:** First, I will not repeat what has been said na ni viziru nizungunze na Kiswahili kwa sababu hakuna mtu wa interpret.

Tungependa sources of rule to be Parliament, Court, President and other legal institutions, hatutaki President ajaye awe anatutengenezea sheria. Msemu kama kutoka leo ninasema hatutaki kuusikia kwa nchi yetu tena.

Loyalty should be to the institution of leadership not to the individual.

Lile neno la Unitary Government and Majimbo ni maoni yangu mimi nikiwa mwalimu katika eneo hili na nimezaliwa hapa ya kwamba ni vizuri tujue tukisema we want Majimbo tunataka nini hasa. My proposal should have been, kwanza tuteuwe kamati ya wale watu educated kwa hili eneo letu la Kajiado North wafanye investigation wajue tuna nini, mapato yetu ni nini? Tukisema tunataka kujitawala do we have economic facilities, do we have returns in this place? Kuna matarajio ngapi tutapata?

At the moment I would advocate for the Unitary System of Government the way it is lakini mapato ya kila eneo kwanza irudishwe kwa hiyo eneo ili ionekane kama ya kwamba watajitegemea. Hatutaki kusema tuwe na Jimbo halafu baadaye tukae kama tuko jangwani, and then what will happen to the facilities that have been contracted by the taxpayers money? Zile rasilimali ziko Nairobi, Mombasa na pahali pengine ambapo tumejenga na taxpayers money tutazifanya namna gani? Kwa hivyo nafikiri kitakuwa kitu ambacho tunatakiwa kukifikiria sana.

Fundamental rights, I will not repeat, they are many they will be read lakini ningependekeza tu kidogo kusema ya kwamba our hospitals zimekuwa ni kama consultation centre unaenda pale unaandikiwa ukanunue dawa pahali pengine. We want hospitali ambazo ziko-properly equipped.

Kitu ambacho tunakosa katika nchi yetu sio Majimbo ama Unitary Government or anything else, it is genuine leadership. Ukiwa genuine ukiwa Mmaasai, ukiwa Mkikuyu, ukiwa nani it does not matter, the system will be perfect hata ikiwa ni nini mradi uwe na moyo genuine wa kusaida raia.

Ningependeza Kajiado North iwe-divided to another may be constituency, ni kubwa, electorates ni wengi. Kama we can get another constituency in this area I will appreciate very much.

Ningependekeza hili jambo la land issue kwa sababu linaonekana it is very sensitive in our country iwe postponed by the Constitution. Tuseme kama kuna Trust Land iwe gazetted, this is Kenya Government land, we give it about 30 years and that time we educate our people properly such that when it comes now to allocation of Government property or land we know exactly what we are saying. We do not want to see a funny situation like what is happening in Palestine. Kwa sababu wakati umeuza shamba yako ulipewa pesa na hizo pesa has time value, tukisema tutatumia historia hatuwezi kutumia historia ya tangu nchi hii ianze. It is a very long history. Those who were there actually they sat down and they came up with something, kwa hivyo hatuwezi kuishi na maishi iliyopita kila wakati,vile iko ni tusimamisha kama kuna mali ya Serikali iwe gazetted hakuna kupeana mashamba, hakuna kupeana plot, hakuna authority to dish iwe gazetted. Kama itapeanwa iwe under Constitution

nyingine lakini hii tuseme no issuing of Government property, hakuna kuuza plots Nairobi, building and all that. When it comes to selling land let it be kept constant for the time being kwa sababu Kenyans are polarised tribewise.

Wakati huu vile tulikuwa hapa asubuhi saa hizi is different, kama mtu angekuja pengine aseme angetaka Unitary kind of Government you could have seen the reaction, it could have been very awkward. Hata Yesu kama angekuja hapa aseme Unitary kind of Government, it could have been very sensitive. Kwa hivyo we are polarised and we have to accept that and we give it sometime in this country.

**Com. Githu Muigai:** Next, that point is taken.

**Joseph Wathigo:** Harambee, 18 months after independence the founding father of this republic observed the following and I quote “we rejected those western capitalism and eastern communism and chose for ourselves a policy of positive non-alignment. We are bound to ask ourselves, where are we going and how we will get there?” The source is Kenya Sessional paper 10, of 1965. Tunatakiwa tujiulize, tangu wakati huo tumefika wapi? Tuko pale pale ama tume-make some steps.

Alitoa mwito wa harambee, the point is harambee, ali-observe kulikuwa na vitu vitatu ambao vilikuwa vinatumiza wakati huo. Wakati huo mimi nilikuwa na miaka mitatu, alisema there was poverty, there was disease.

**Com. Githu Muigai:** I am sorry I will have to ask you sir, you see we have to break at 5.00 p.m. We have 15 people who have not spoken, please identify a problem and then give the solution. Harambee is being abused, solution, abolish and then we move on, please for the sake of those who have not spoken.

**Joseph Wathigo:** Sawa kabisa. Harambee zimekuwa ni jukwa ya kutukanana, ukitaka kutukana mtu unaitisha harambee halafu unaanza kumtukana, unatakiwa iwe-streamlined. Imekuwa ni kama kitu cha kujitajirisha, ukitaka kuanzisha kitu, unakuta siku hizi kuna vitabu kwa maofisi before you do anything you have to contribute. Kwa hivyo harambee imekuwa misused na tungetaka kama inatolewa iwe properly accounted for.

Lastly, Commissioners I have documents which will be read but tungetaka Serikali yetu ijayo iwe Serikali ambayo ina-create employment, feed the population and empower the population kwa sababu tukiwa matajiri, hii mambo ya shamba hatutakuwa tuKizungumzia.

Politicians should not invest outside the country. Wakati wanaweka pesa nje wanaenda mtu ananunua nyumba outside ni kama kusema anatarajia kuishi maisha mengine upande ule kwa hivyo kama ni true politician, a-invest hapa na atuonyeshe good example.

MPs should not engage themselves in physical business, the package is good now and the results should be expected.

The Government should not govern through trial and error method. Vile mlikuwa mmesikia uchaguzi utakuwa next years, sasa leo gazetti ya leo umesikia ni leo. Tunataka firm things kama ni wakati wa uchaguzi uwe fixed, kila Mkenya ajue na aanze ku-plan according to that date.

Electoral Commission should be set by Parliament.

Lastly, dear Commissioners it is my request to you to know that this country lies in your hands at the moment, we want you to stand as counted people in this republic. One day we want to say Githu Muigai came to Ngong' and we gave him our wishes and this is why our country is featuring well. We want to compete with other countries, we do not want to remain behind.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana. Thank you very much for your views kuna swali moja tu, one munute.

**Com. Wambua:** Commissioner Muigai and Commissioner Wambua anyway, do you want to have this Constituency split into two before the next general election?

**Joseph Wathigo:** That is true.

**Com. Wambua:** That is how you want it. We wish you every luck in the forth-coming elections. Thank you.

**Joseph Wathigo:** Thank you.

**Com. Githu Muigai:** Thank you. Mzee sasa ni wewe halafu tafadhali tukubaliane wazee wale hatujazungumza mtu akisimama hapa anasema yale mambo ambayo tumeona si mazuri ni hili na hili na hili na masuluhisho yetu ni hivi na hivi, na hivi ndio tusihadithi sana kwa sababu kutoka asubuhi tunaelewa sasa historia yote ya Kajiado North. Tumekubaliana? Tafadhali, dakika mbili mbili.

**Onesmus Gathija:** Commissioners asante sana kwa kuja kwenu, mimi kwa majina naitwa Onesmus Gathija Gadungo. Mimi nitaongea mafupi kwa sababu mengi yametajwa, nitaongea kuhusu elimu.

Tunashida sana, tuna watoto 'chokora', kama hapa Ngong' wamejaa wanavuta gum and I think it is the whole of Kenya. Ningeomba Serikali itafutie hawa watoto mahali, wakishikwa wanapelekwa kwa shule kwa nguvu kwa sababu hawa watoto ndio wanatupiga usiku. Tuna watoto yatima, watoto wazazi wao wamefariki kwa sababu ya huu ugonjwa wa Ukimwi, pia

tungetaka hao watoto watafutiwe masomo ndio tuone kama wanaweza kufaidika.

Pili ni kuhusu hospitali, kuna hiki kitu kinaitwa cost-sharing, tungeomba Serikali hii cost-sharing iondolewe kabisa kwa sababu kuna akina mama wakongwe yaani wale wazee kabisa, grandmothers na vile wako vijana mnajua siku hizi watu wengi wametupa mama zao. Unakuta mama mkongwe peke yake, ni nyanya mzee, vijana wako kando kando, huyu mama akienda hospitali hawezi kutibiwa anaambiwa kwanza alipe pesa ya kadi halafu aandikiwe dawa, huyu mama atatoa pesa wapi? Hakuna, kwa hivyo tungeomba Serikali hii Katiba mpya tunatengeze wa-scrap hiyo cost-sharing.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumesikia, tuende mbele.

**Onesmus Gathiga:** Tatu ni kuhusu Judiciary, kuna shida kwa watu maskini katika Kenya vile tuko siku hizi. Kuna shida kwa sababu ukiwa huna pesa umenishitaki na kunipeleka kortini unaleta wakili, mimi sina nguvu za kushika wakili, mimi wakili wangu ni Mungu, unasikia nimetumbukizwa Kamiti, nimekaa huko miaka kumi nakufia huko.

**Com. Githu Muigai:** Pendekeza, ungelipenda sheria ifanye nini?

**Onesmus Gathiga:** Ningependa sheria watafute kama ni mtu maskini na hana uwezo na yule mtu anahitaki yeye ako na uwezo, hata Serikali iwe inatafuta wakili wa kusimamia huyo maskini naye awe akimtetea kama tajiri anayetewa na wakili wake.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo ni mzuri tumeandika, anaitwa public defender.

**Onesmus Gathiga:** Very good.

**Com. Githu Muigai:** Tumeandika hiyo, asante sana.

**Onesmus Gathiga:** Nne, kiko kitu kinaitwa divorce, divorce imekuwa shida katika Kenya kulingana na hawa akina mama wanaoiwa FIDA, hawa akina mama wanaotetea akina mama. Wazee hawana mtetesi.

**Com. Githu Muigai:** Pendekeza.

**Onesmus Gathiga:** Bibi unaoa yeye mnazaa watoto wawili halafu anatoroka, anaenda anaolewa pahali pengini, anatoroka anaenda pahali pengine anasema huyu ni bwana wangu wa zamani, anawacha watoto wanataabika. Kwa hivyo tungeomba Serikali mambo ya divorce waangalie kabisa wazee wasije wakaumia, hii FIDA imeumiza wazee.

**Com. Githu Muigai:** Wazee wananyanyaswa?

**Onesmus Gathiga:** Waangaliwe.

**Com. Githu Muigai:** Waangaliwe?

**Onesmus Gathiga:** Asante nimemaliza.*(Laughter)*

**Com. Githu Muigai:** Asante sana, wazee wasaidiwe pia. Okay, anza na jina lako. Tafadhali tafadhali tunyamaze, anzia kwa kutupatia jina.

**Caleb Ambogo:** My names are Caleb Ambogo Mwa.

**Com. Githu Muigai:** Wananchi watukufu tafadhali mnyamaze. Basi endelea.

**Caleb Ambogo:** My names are Caleb Ambogo Mwa.

**Com. Githu Muigai:** Yes Bwana Caleb.

**Caleb Ambogo:** There are some areas I am very sorry to mention because target ya Kenya thereby leaving wananchi aside, we are the sufferers.

Early marriages, many school leavers in Kenya today are involved in early marriages and the future of their children is bleak these children become 'chokoras'.

**Com. Githu Muigai:** Caleb, we agreed here this morning that early marriage is wrong, solution?

**Caleb Ambogo:** I proposing that the Government should take care of the school leavers.

**Com. Githu Muigai:** Okay, Caleb anasema wasichana wadogo wasiozwe kabla ya kumaliza shule hiyo inaharibu maisha yao.

**Caleb Ambogo:** Another point is concerning the registration of Churches, we have many denominations in Kenya today, some are not (...Inaudible) to the community. I am proposing that the Government should take care of the many denominations that are coming up. Concerning the Church too we would like to know the day of worship because this is like business now, people are just coming from nowhere because they are using wananchi, wakitaka pesa. We should select the day of worship.



**Com. Githu Muigai:** Tumeelewa.

**Caleb Ambogo:** Another one is concerning health, we have qualified doctors in Kenya but their work is being interfered with by nurses. The nurses are wasting a lot of time, wanafanya kazi ili ifike jioni waende nyumba lakini wagonjwa wanateseka sana kwa sababu hakuna taratibu ya kufuata. Kuna wakati wa kuona daktari wanasema kwa saa moja patients watatu, kama ni wakati wa kuona daktari mgonjwa ni mgonjwa, he is supposed to see the doctor ili apate dawa.

**Com. Githu Muigai:** Na kwa hivyo tufanye nini?

**Caleb Ambogo:** Napendekeza nurses should not ...(incomplete)

There is another thing concerning population, in Kenya we are talking about finance, lack of money, employment etc. We are the people who are causing such problems, each parent should have 3 children, the birth rate should be standardized.

**Com. Githu Muigai:** Mzuri,asante sana Bwana Caleb. Umebakisha?

**Caleb Ambogo:** Namaliza na mambo ya 'chokora' we have a responsibility as a result of girls who give birth early, the Government should provide a home where these children are taken care of and the Government should also look for ways of controlling this.

**Com. Githu Muigai:** Okay Caleb, tumeshika hiyo asante sana.

**Caleb Ambogo:** We have married and unmarried women in Kenya nowadays, and I want to concur with my colleague who proposed that the women population in Kenya now is very high, how can one man get four wives?

**Com. Githu Muigai:** What is your proposal.

**Caleb Ambogo:** There is polygamy and non-polygamy.

**Com. Githu Muigai:** Caleb, jiandikishe hapa. You have said that we should encourage polygamy because there are too many women and very few men. In the circumstances where a man can one be able to take care of his wives but the one who cannot take care should not. Okay, it is very clear.

**Simon Simiyu:** My names are Simon Simiyu. Mine is strictly on education, the system of education we have is confusing and leaves a lot to be desired. Reason, the 8-4-4 system of education has failed to address its intended purposes. We know very

well that the purpose of ushering in the 8-4-4 system of education was to strengthen or to go into technical education. Looking at it now the way it is, all the subjects that would make features of the intended purposes have been faced out and therefore I propose that the whole system be scrapped or abolished and be replaced by 7-4-2-3 system along side with technical schools the way it used to be.

On the line of technical schools, I again propose that every district to begin with must have a technical school. A good example is where we had Kabete Technical School, Kaiboi and so on just to mention a few.

**Com. Githu Muigai:** Mr. Simiyu once we give the principle tutaita waalimu halafu they work out the details. Another point?

**Simon Simiyu:** Secondly, I also propose that for any curriculum should not be allowed in our primary schools especially from class one to standard eight, should not be subjected to any curriculum because we to want address the issue of our nationality.

Thirdly, the quota system currently in use should be abolished, reason for me to day that, we are breeding the type of students who do not know anything about their country. Here is a child who has been educated in Ngong' possibly primary, secondary Ngong', College perhaps Ngong' and after that, if he or she is a teacher she may be posted to teach in Ngong'. What does this teacher know about Kenya? Therefore, students should be allowed to be admitted in schools nationally and in all provinces in Kenya, from Ngong' let the child go to West Pokot or Turkana.

**Com. Githu Muigai:** That point is well made Mr. Simiyu, tunakubalina na hiyo yaani Kenya yote wanafunzi wote watembee nchi yote ndio tuwe nchi moja na watu wajuane na mila za wenzao. Hiyo tumeshika, next point?

**Simon Simiyu:** My forth proposal is that, there is need for the Ministry of Education to revive Kenya School Equipment Scheme. While we are crying that our children are not able to undergo learning or education it is because of this minor facilities like books and stationery. These things should be provided the way we used to have them in the past.

Lastly, may I also touch on the question of politics now, I propose that on the issue of nomination of MPs and Councillors, let political parties not be allowed to have a role in nomination but instead the 12 seats be reserved for interested parties like the disabled, where by we can have 2 representatives from the blind, 2 representatives from others with other deformities. Then the gender issue should now come in, we can have 3 representatives from women section and so on. I think that one will be more important than allowing MPs or these political parties to nominate the 12.

**Com. Githu Muigai:** We have heard you on that one. Next?

**Simon Simiyu:** Thank you that is all I had.

**Com. Githu Muigai:** Thank you very much. Mzee tumekufikia wewe tafadhali tusonge hivi. Kuna mtu yoyote angependa kuzungumza na hajaitwa? Ukaribie.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Ore taa nanu kara taa olkeek onyokiei.*

**Translator:** He is from Kerikonyike section. *Kaji tii imbungu imbunga ake iyie kuna neijia ene.*

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kara taa olmaasani lo payiani kuldo oyautua Katiba.*

**Translator:** And he is a Maasai by tribe.

**Com. Wambua:** Did we get the name? Jina?

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kanyor taa amu kaning oshi ake Katiba.*

**Translator:** He is so grateful because he has been hearing about the Constitution.

**Com. Wambua:** Excuse me? Ametaja jina?

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kaisetie ole korikoro.*

**Translator:** His name is Kaiseye ole Korikoro

**Kaiseye ole Korikoro:** *Natonita te nkop naji olosho oibor.*

**Translator:** And he is from Oleshebo area.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Abori tene Ngong.*

**Translator:** Just beyond Ngong' hills.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Naaajo ashe Katiba iyiewuo.*

**Translator:** He wants to thank you the Commissioners.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Amu kaningoo oshi ake te die te idie najo kanu Kenya ebau.*

**Translator:** Because he has been waiting for you for too long.

**Com. Wambua:** I can not hear properly and also explain to him that we do not have a lot of time, we are closing at 5.00 p.m. it is only 20 minutes to go, let him give us the problem and the proposals so that we can move faster.

**Translator:** *Etejo ore taa iroro naa point, point amu ildakikani tikitam kiata neton engor kulikae tunganak.*

**Kaiseye ole Korikoro:** *Ore taa duo naaduo natejo iladuo maasai oyetuo ore ina kiunga mkono kira ilmaasai.*

**Translator:** He is in support of all the other Maasais said.

**Com. Wambua:** All what the Maasais said, the ones who were in shukas, the ones who were in ties, he supports them completely, Federal system, land problem, everything. Does he have anything else to add?

**Kaiseye ole Korikoro:** *Nalotu imbaa are ake .*

**Translator:** He has got only 2 points to make.

**Com. Wambua:** Let him add those two points.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Naa katoninguo duo ina taabu natii ene.*

**Translator:** He is going to analyse the problem.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Ore entoki e taabu o ilmaasai oleng.*

**Translator:** The biggest problem in Maasai land is,

**Kaiseye ole Korikoro:** *Naa soko nmirie inkishu enye*

**Translator:** Is the market for their livestock.

**Com. Wambua:** That was mentioned this morning.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kiata apa to kireza too kuda olongi ake ewuei neji KMC.*

**Translator:** We had KMC even during the colonial days.

**Com. Wambua:** Just hold on, tell him that we have already recorded that the Maasai want 1, a Ministry of Livestock, 2, they want the equivalent of KMC and it should be located in Maasai land, that has been recoded.

**Translator:** *Kidipa duo atoning inchere keyieu .*

**Kaiseye ole Korikoro:** *Aia kaimaa ake naa inatoki apa naishu iyiook taabu.*

**Translator:** Our problems will be over once we have a market.

**Com. Wambua:** Let him tell us the second problem.

**Translator:** *Nalotu enewueji.*

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kiata ilarikok oshi taata egeluni.*

**Translator:** We have our elected leaders.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Etai ilaguanak etai ildioni.*

**Translator:** We have the administration including the Chiefs and the Dos.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Naa kalotu entoki natiene.*

**Translator:** And he would like to know only one thing about the administration.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Eji ore chifui tene geluni naa ilarin onom omiet eishu.*

**Translator:** Once a Chief has been appointed, he will be in that office until he is 55 years old.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Naa ore osiasai naa naa nkolongi ake eikenuni ilarin imiet.ake nidol etanangayioki.*

**Translator:** But a politician should have one term or two terms if he is lucky.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Najo sii toi olbungei otii dukuya olikae.*

**Translator:** And I think a Member of Parliament is more important than a Chief.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kaji di etiu pee eeta ninye ilarin kumok nemeeta elde.*

**Translator:** Why should a Chief have 50 years in services?

**Com. Wambua:** Exactly, does he want us to elect them, let him just say Chiefs and Assistant Chiefs should be elected so that we record it.

**Translator:** *Kaa eyieu neikoni.*

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kayieu naai neingurari ena .*

**Translator:** He wants that thing to be checked *Eyieu iyie niaku ilarin aja ebik olchifui.*

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kayieu nanu naa ore te duaata ai*

**Translator:** According to him.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Mme palayu duo ilarikok itu engeluni.*

**Translator:** It is good to have leaders.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Kake kayie u naai naa ilarin matikitam o imiet sii ninche eishu nedotuni.*

**Translator:** But let a Chief not exceed 25 years in service.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Nalotu enkiti wuei netii ene pee alo aton.*

**Translator:** He has another point here.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Etai iltunganak oota taama ,taama enkop olkulikae.*

**Translator:** There are people who crave for other peoples' land.

**Kaiseye ole Korikoro:** *Ore ina temaa engoru irara ilarikok eninkoko amu kajo sii duo ore kipuo eda kukuo naa kuna mbaa intobiritata.*

**Translator:** The Constitution should protect those whose land has been grabbed.

**Com. Wambua:** Mzee, register. What did he say, the last portion? Haya next? Taja jina mzee na uendelee hapo haraka haraka.

**John Kulei:** Mimi nitaongea kwa Kiswahili.

**Com. Wambua:** Haya endelea.

**John Kulei:** Mimi ninaitwa John Kulei.

**Com. Wambua:** John, haya endea.

**John Kulei:** Kutoka Ngong' lakini mambo yangu ni mafupi tu kwa sababu mafuta yote imenyonywa.

**Com. Wambua:** Ni kweli na imeingia kwa machine, imenaswa. Kwa hivyo taja yale ambayo hiakutajwa ndio tumalize.

**John Kulei:** Nataka kuongea kuhusu shule, Chifu na yametajwa yote.

**Com. Wambua:** Kwa hivyo unataka?

**John Kulei:** Mimi pendekezo langu ni watu wawe huru na amani na wawe wakijiulizia mambo yao kama vile nimesikia kuanzia asubuhi, mambo yao ya uhuru.

**Com. Wambua:** Hiyo imeingia kwa machine mzee.

**John Kulei:** Kama vile mini ni Chairman wa district kama Kajiado wa Mau Mau katika Kenya na nimefurahi sana, imependekezwa hivi ikisemekana kwa sababu sisi tuna 42 districts and vile mnasema Majimbo. Nimesikia uchungu kwa vile mmesema Majimbo na mnataka mashamba zile zilikuwa za Wazungu, na hiyo ni kama tunaigilia sana ile Tume ya Njonjo. Sasa nauliza Wamaasai wetu, tukiwa na Majimbo kile kitu tutafuata na njia gani? Kwa hivyo ...

**Com. Wambua:** Basi fanya proposal.

**John Kulei:** Pendekezo langu ni kusema uhuru, kama vile hawa watu walikuwa wanapigania uhuru wenyewe, walikuwa wanapendekeza vitu vyao wapewe.

**Com. Githu Muigai:** Tumekusikia mzee na tumeandika yote. Asante sana tumekusikia. Haya mwenzako, hiyo tumesikia.

**John Kulei:** Wacha niseme moja tu.

Ningependa kama vile watu wameongea kuanzia asubuhi, mapendekezo yao tuwe kama vile tulifinywa na wale watu walitupiga wakati wa ubeberu. Wawe wanauliza vitu wakiwa-free na warudishiwe kama vile tunafuata. Tungependekeza maskini kama vile tunateta huko, maskini wale wasio na nguvu kwa sababu Serikali hii yetu imekuja mpaka ikawa kuna wale wengine kama wakoloni...

**Com. Githu Muigai:** Mzee, hiyo sasa tumekusikia, umetoa points mbili za maana sana. Uhuru na umoja wa watu wa Kenya, tumesikia, imechukuliwa kwa tape na tumeandika. Hawa wazee wanzako lazima wazungumze kabla hatujafunga saa kumi na moja, wapatie heshima hiyo. Asante.

**John Kulei:** Yangu ya mwisho, moja tu.

**Julius Kuraru:** Niendeleo? Kwa majina naitwa Julius Kuraru na ningependa kushukuru Commission kwa kuweza kuja kuchukua views zetu siku ya leo. Tumekuwa tuingojewa na ni furaha yetu. Sina mengi, nitapitia tu kidogo.

Ya kwanza ni juu ya title deeds ambazo zimetajwa sana, mimi ningeeunga mkono iwe ni ya familia yote mzima kuanzia baba, mama na watoto vile wanavyo ishi kwa nyumba ama vile wanavyoishi ndivyo title inakuwa kwa majina hata watoto kama ni kumi wote wawe included.

Ya pili, nikija upande wa Parliament ni kwamba wananchi wapewe uwezo ama kungekuwa na sheria itakaowatia uwezo

kuweza kumtoa Mbunge yeyote ambaye hatimizi hata ahadi zake ikifikia. Kama Mbunge wa miaka miwili anapokuwa amechaguliwa Bungeni na aweze kutupwa nje na mwingine kuchaguliwa. Nikiwa tu pale kwa Bunge, wananchi wangepewa uwezo zaidi wa kuweza kupiga kura ya maoni kabla Bunge haijapitisha chochote kama vile vile tumeona juzi wakipitisha mambo mengi ambayo yanatushangaza.

Langu la tatu, ni kuhusu mavazi kwa akina dada, ningependa sheria ibuniwe hasa katika enzi hii ya ukimwi itakayosimamia mavazi haya tunaita modern dressing. Kwa sababu tunaona wadada wetu hivi karibuni wataenda uchi na tusipokuwa na sheria ya kusaidia hiyo tutakuwa na shida nyingi hapo baadaye.

**Com. Githu Muigai:** Akina dada wavalishwe vizuri na sheria, tusonge mbele.

**Julius Kararu:** Langu la nne, ni kuhusu sheria ya makanisa, sheria hapa inatuambia kwamba kuna uhuru wa kuabudu lakini uhuru huu wa kuambudu inaonekana tumeuharibu na sheria ingepatikana ya kuweza kusaidia makanisa ili tusiwe na wakora ambao wanaweza kujitua wao ni wahubiri na huku wanakuja hata kunyanyasa wananchi ambao hawajuhi hata ukristo ni kitu gani. Pia nikiwa pale katika upande wa Kanisa, kungebuniwa hiyo sheria ambayo ina-state ama inaonyesha wazi kwamba sisi tukiwa WanaKenya tuko-supposed kuabudu Mungu ama ni shetani. Kwa sababu sheria haionyeshi vizuri hasa tuko-supposed kuomba nani.

Langu la mwisho ni kuhusu wanajeshi wetu, tumeona ufasidi mwingi ukifanywa katika nchi hasa kwa upande wa ujenzi na wanajeshi wetu wengi wana hiyo manpower na wana idara ya kufanya kazi kama hiyo. Ningependa kama sheria ingebuniwa itayowawezesha wanajeshi wetu wahusishwe katika miradi ya ujenzi katika nchi hii yetu na kutuletea mfano mzuri wa kuweza kumaliza ufasidi katika upande huo wa ujenzi. Nashukuru, ni hayo tu.

**Com. Githu Muigai:** Ngoja kidogo kuna swali moja.

**Com. Wambua:** Excuse me, you said that there should be a referendum before the Parliament passes anything. What would be the role of Parliament? Why then elect them or are proposing that certain fundamental issues must be subjected to a referendum before Parliament passes them, because there is no point electing MPs if you are saying before you pass anything you have to bring to us?

**Julius Kararu:** Ningependa kusema ya kwamba, hiyo Constitution iwe amended kwamba kuna issues ambazo zinahusu hasa wananchi kama vile wakipitisha mambo mengine ambayo yanahusu wananchi kwa undani zaidi, warudi huku kwetu kama vile walivyopitisha mishahara, walivyopitisha wapate bunduki. Wanafaa warudi hapa kwetu tuwaambie ndio ama la.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana. Mama, uanze kwa jina tafadhali ndio tuipele kwa tape.



**Esther Gathoni:** Jina langu naitwa Esther Gathoni na mimi ni mkaaji wa hapa Scheme 305 lakini yangu nataka tu kuongea kutoa pendekezo straight away. Nilikuwa napendekeza ile Serikali tutapata ifikirie sana maneno ya street boys na street girls. Zamani wakati wa wabeberu tulikuwa na approved schools na ilisaidia sana, hawa watu tutashidwa kuwa-control. In another ten years hata hakuna mtu atakuwa akitoka kwa nyumba.

Ya pili, nataka kuongea maneno ya strikes especially ya hospital na buses, zile vitu raia wanatumia ndio wapate daily bread. Kama hospitali kuko na taabu, kama Serikali hii inaweza wakati ule madaktari na nurses wana-qualify wawe waki-sign maneno ya strike because wakati ule wana-strike tunapoteza nyoyo mingi sana hospitali, na sioni kwa nini wale watu wanakuwa kwa kazi wakati huo hawawezi kuwa-charged na murder like any other person yule anaenda anaua mtu kama amegonga na gari ama kwa kitu kama hicho?

Ya tatu, ni ya ku-protect personal dignity kama sasa vile unafanya kazi yako hapo unaweza kuleta taabu kidogo in the process of your work. Kitu kama hicho hata kama ni magazeti iwe na protection because wale mnafanya kazi hii ya Serikali mko na familia na mabibi na wazazi. Sometimes it becomes very embarrassing, tuone kwa hii Constitution mpya ile heshima tutapatia wale watu wanatufanyia kazi hata kama kitu kimetokea. Asante sana.

**Com. Githu Muigai:** Thank you very much mama hiyo point yako nitakuambia tumeenda mpaka Garbatula hatujaisikia, ni ya maana sana.

**Joseph Gitau:** Thank you very much the Commissioners who are here, by name I am Joseph Gitau from Kajiado North, this is where I stay in Ngong. My first point is about the youth. I am proposing for the new Constitution, the present youth to be involved so that they can have a national cake from the Government. Right now as the youth right now we are the ones who are so poor, for example, like me I am a family man with a wife but my father cannot allow me to have a share of his own property. The Government is still following the same system and cannot allow me to have the national cake. Where are we heading to, because that is why when the politicians come to us and give us some small token of money, they say shikeni kitu kidogo lakini utapata wapi hiyo kitu kubwa?

**Com. Githu Muigai:** Make your proposal. Are you suggesting that before your father dies he should give you your own property?

**Joseph Gitau:** I am proposing that we have a policy in the Government that I am entitled to the national cake inform of loans naweza kupatiwa loans za ku-maintain familia yangu na nitailipa kidogo kidogo.

The other thing is about the forests, mnaona saa hii hakuna misitu, it is my proposal that the Chiefs as the Government agents

who are near the people they should be given more powers so that they can protect the environment, because the rate at which our forests are being destroyed and reduced to the size of the republic of Togo.

The other thing is concerning the Police, can you imagine somebody who is working day and night analipwa Kshs. 5,000/= na security man of EAS company is getting Kshs. 15,000/=. We should have better housing for the policemen so that they can work, wanatufanyia kazi mzuri. Hawatahitaji kitu kidogo wakiangaliwa vizuri, but a hungry man is an angry man so as far as I am concerned, I am supporting the Policeman and other Government employees to be given better housing facilities and fringe benefits so that they can offer better services.

Another thing, we should have accessibility to good water, fresh water, the Government should dig boreholes. Right now in Ngong we do not have any borehole. Mimi nilipozaliwa nilikuta hakuna maji na pengine nitakufa niache hakuna maji.

**Com. Githu Muigai:** Maji kabla hujakuja, tusonge kwa point nyingine. Asante sana.

**Daniel ole Wantia:** Basi kwa majina mimi naitwa Daniel ole Wantai na nimetoka Kikonyeki South. Basi mengi yamesemwa na kwa sababu hatuna nafasi na naona ndugu zangu hapa wanapenda akutoa maoni sipendi kurudi nyuma napenda kuenda mbele, naongea moja, mbili halafu nawaachia nafasi.

Upande wa kortini, kama vile mwenzangu mmoja alivyosema hapa na alisema kitu cha muhimu sana. Ukiangalia upande wa korti kuna watu wengi maskini ambao wanachukua kesi zao katika korti hasa kesi ya shamba. Pengine wanagombania shamba sehemu kidogo ya shamba na wanagombania na mtu fulani na kuna mtu ambaye hana uwezo yule wanabishana naye katika kesi ya shamba hilo. Huyu maskini akienda kortini hana haki hata kidogo lazima ataangushwa hata kama shamba hili ni lake. Kwa hivyo mimi nataka kuomba commission hii yetu mkienda kuunda sheria, muunde sheria ambayo italinda kila mtu ambaye ako na ukweli. Kama sasa ukiona mashamba zinakatwa na ile kamati ambayo yanakatia watu mashamba iwe ndio watapewa jukumu ama watapewa uwezo wa kuweza kuamua kesi kama hizo za mashamba kortini ili ukweli ipatikane.

Pamoja na hayo, mimi nataka kurudi nyuma tu kuguzia kitu kimoja ambacho ilisemekana hapa asubuhi kwamba machifu wachaguliwe na raia. Ukiangalia ile Serikali ambayo iko karibu na raia ni machifu. Machifu wanapochaguliwa wanachaguliwa kwa kipendeleo, watu wanaenda kukaa kwa ofisi, wanasema tupatiwe fulani kwa sababu ni tajiri, utupatie fulani kwa sababu ni mtoto wa tajiri. Sasa hapo hawajachagua uhuru, wananchi wapewe wachague machifu ili tupate machifu ambao watafikisha masilahi ya raia. Sina mengi ni hayo tu.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana, tusonge mbele mzee.

**Joel Yamo:** Asante sana ma-commissioners ambao wameweza kufika hapa kwa kupata nafasi hii ya kuzungumza kidogo.

Kwa hakika mengine nitakayotaja hapa yatakuwa labda yamezungumzwa lakini kwa vile nimekaa hapa sana naona tu nitayazungumzia.

Kwanza kabisa itakuwa ni...

**Com. Githu Muigai:** Anza kwa jina tafadhali.

**Joel Yamoi:** Majina yangu ni Joel Yamou Paing'oni. Mimi ni mkazi wa hapa, area hii ya Ngong, Location ya Ololwa, mahali inatwa Kerarapol, mwanzo wa Kajiado District mahali ambapo tumezungukwa na forest. Kuhusiana na mambo ya misitu katika Kenya kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa misitu katika Kenya. Jambo hili linaweza kutatuliwa tu kama kungeweza kuwa na more community participation katika misitu ile iko karibu na wao. Kwa njia gani? Hawa watu wapatiwe nafasi walime chini ya hii misitu, sheria itengenezwe na Serikali pia nayo ipeane miche ya kupanda katika forest. Wewe ukikutwa sehemu ile ulipewa imekauka miti hautapewa nafasi ya kulima tena. Miti ikisha-mature then Serikali inaweza kujua vile itakavyoweza kuuza hii miti maanake kutazuia uharibifu wa misitu zaidi.

Tukija kama ni kuinua jamii ya Kimaasai kiuchumi, hakuna jambo lingine ambalo linaweza kufanyika bali kuwajengea slaughter houses nyingi kushinda vile kuko sasa. We have a case study of a very small country called Botswana na it is mountainous. Leo hivi Botswana is one of the richest countries in the world kwa udogo wake na mapato yake inatoka wapi? Mapato yakeyanatoka kwa ngombe tu kama hivi za Wamaasai hapa, ni kwa sababu kuna njia mzuri ya kufanya marketing ya nyama kwao. Sasa ukiangalia Maasai akipiga ngombe kutoka Mosro mpaka Dagoreti, huyo ngombe amepoteza ratili, amekwisha njiani.

**Com. Githu Muigai:** Pendekeza mzee?

**Joel Yamoi:** Nambari ya tatu ni juu ya Land Control Board, hizi Board zimekuwa ni daraja ya kufanya jamii ya Kimaasai kuwa maskini kabisa. UKizunguka hapa Ngong peke yake uone watu waliokuwa na mashamba makubwa makubwa, watoto wao sasa wamekuwa mere penpers beggers and some of them have become very useless.

**Com. Githu Muigai:** Mzee sitaki kukukata kabla ya kumaliza lakini asuhuhi tulizikizana kabisa mambo ya Land Board, watu wote tukasikizana kwa hivo usiongeze chumvi zaidi ya hapo.

**Joel Yamoi:** Sasa ile nyingine imezungumziwa lakini nitaongeza point moja. Wamaasai maisha yao yote wamekuwa, hawa watu walizungumzwa kutoka Mt Elgon mpaka kule kwote walipita sizungumzii sana hiyo ni historia. Serikali baada ya hii Katiba kuisha, isaidie Wamaasai kupata a legal representation, lawyers ambao watastaki British Government iweze kulipa Wamaasai vile ilivyowasumbua mpaka sasa kuwasukuma pande hizi kuwatoa zile areas zilikuwa safi. Maanake hii haitasikizwa

mpaka jamii ya Wamaasai ishitaki the British Government.

Jambo la tatu ni juu ya orphans ambao wanawachwa siku hizi kwa wingi sana na huu ugonjwa wa ukimwi na nja zingine. In fact hawa watoto wamekuwa hawana mtu anashugulika na wao na unakuta ya kwamba hata kama wazazi wote wawili wamekufa huyo mtoto anakuwa dis-inherited na wale members wengine wa familia. Sio kusema ati sababu wamekufa huyo mtoto hafai kurithi ilei mali ya baba yake. Kutafutwe sheria ya kulinda watoto kama hawa.

Boarding schools zijengwe zaidi katika nchi ya pastoralist community. Hebu fikiria hivi leo, unasikia mtoto ametoka mahali kama Mosiro, amechukuliwa secondary school, good, lakini amechukuliwa wapi? Keviko Day School ama Ololwa, atakuwa anatoka Mosiro kuja day school hapa? Kwa hivyo hata wakati kunafanywa selection ya secondary schools, jamii hizi za pastoralists, watoto wao wawe wakiangaliwa wachukuliwe boarding schools sana na Serikali ijenge more boarding schools kwa communities hizi ambazo zina-pastoralists. Hii ndio njia moja ya kuweza kupigana na kutojua kusoma katika Maasai community. Ni masikitiko makubwa sana kukutana nao wakati wanahama wakienda upande wa Ruiru, unaona watoto wadogo nao tuko nyuma. Badala yake hao watoto wangeachwa kwa boarding school wakisoma wazazi wahame waende kutafutia ngombe zao malisho. Serikali ichunguze sana hili jambo la kujengea Wamaasai boarding schools na hasa ziwe separate, girls boarding schools ili wasichana wa Kimaasai waweze kuelezwa zaidi juu ya yale mambo ambayo yanazuiya kusoma.

Tukikuja katika ukulima, jamii ya Kimaasai inafaa ifundishwe agriculture zaidi na kuwe na more demonstration farms in Maasai land za kuwafunza njia tofauti za kutumia shamba, sio tu ngombe lakini kuwe na njia za kulima. Hii ni nchi inaweza kutoa vitu viingi sana, cotton, njugu karanga na zingine. Waweze kuelezwa kulima hivo vitu na kupewa loans ndogo ndogo za kununua mbegu na vinginezo.

Lazima pia wafundishwe juu ya civic education maana wametumia kwa muda mrefu sana kwa kutoelewa.

Katika hii national issue ya freedom of worship, this freedom of worship in Kenya where it is enshrined in the present Constitution iwe controlled. In fact imekuwa tena ni njia moja ambapo wahalifu wameweza kutumia hili kufanya mambo machafu sana. Wale mliangalia gazetti leo mliona visa vya masikitiko ambavyo vinafanywa na watu wanajiita mapastor.

Sasa ya mwisho ni juu ya hawa watu wanaitwa rapists na kuna watu wametaja canning iondolewe Kenya. Mimi ningengeza zaidi, viboko viongezwe sana kwa watu kama hawa. Imagine if it were your daughter who has been rapped by a mad man like that one, hata wewe ungetoia apigwe viboko si ni kisu tu ungetoia umkate kate?

Tuje kwa mambo ya ma-plot ambazo zinapeanwa kiholela holela sababu ya tamaa ya pesa. Hebu angalia kama hapa Ngong, hakuna mahali imetengwa ma-industries, watu wanajibandika hizi maplot wananunua.

**Com. Githu Muigai:** Pendekeza, kwa hivyo unapendekeza nini?

**Joel Yamo:** Ningependekeza any public land kabla haijapewa to individuals kukatwe area ya industries na kutafutwe investors wale wanataka, na wapewe bure waonyeshe njia ya kile kitu anataka kujenga. Hii ni njia moja ya kumaliza ukosefu wa kazi.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumeelewa.

**Joel Yamo:** Ningesema mengi lakini Commissioners ninashukuru sana kwa kunipa hiyo nafasi ya kusema hayo machache.

**Com. Githu Muigai:** Asante. Wazee tusonge mbele, dakika tatu tatu.

**John Watari:** Kwa majina mimi naitwa John Watari, nitaenda mbio mbio kwa sababu naona muda hauturuhusu. Ningependa kuelezea kwa kirefu lakini naona haitawezekana tuko wengi sana. Kwanza kabisa nawashukuru Commissioners kwa kazi yenu njema kwa kukubali kutosikiliza mpaka pengine naona karibu saa inapita.

Naongea kwanza juu ya hukumu ya kifo, pendekezo langu ni iondolewe na badala yake iwe hukumu ya kifungo cha maisha kwa wale wanafanya kunajisi akina mama na wasichana na pia wanyanganyi kwa kutumia nguvu. Kwa sababu hii hukumu ya kifo kama nchi yetu ni nchi ambayo inadhamini Mwenyezi Mungu basi ni kinyume na mambo ya kutoa uhai wa mwingine. Kwa hivyo ningependekeza iwe hukumu ya maisha kwa wale wanatenda mambo kama hayo, kunyanganya kwa nguvu na kunajisi.

**Com. Githu Muigai:** Tumeshika tusonge mbele tafadhali.

**John Watari:** Kufungwa gerezani kwa kiongozi yeyote anayeharibu au anatumia fedha za kundi lolote analoongoza yaani mali ya uma, baada ya kupatikana kama ametumia pesa ya uma au za chama chochote na hapo kufutwa kazi na kuachiliwa, awe akifikishwa mahakamani na kufungwa.

Tatu, Mkenya yeyote aruhusiwe kuishi mahali popote na kumiliki mali mradi tu iwe amefuata njia ambayo ni halali si kwa njia ya unyanganyi.

Nne, mishahara ya Polisi isiwe chini ya shilingi elfu kumi kuanzia Serikali ijayo. Wawe wakiongezewa mishahara lakini basic salary iwe shilingi elfu kumi maana tumeshuhudia pengine, tunashuku kwamba wameingilia uhalifu kwa sababu ya malipo duni na wanashirikiana na wakora kutuhangaisha. Pia wawe wakihamishwa baada ya miaka miwili au chini ili wasiwe na nafasi mzuri ya kuzoena pengine na watu wa area ile, maana hii pia inachangia uhalifu. Kabla hajajuana na watu wa area hiyo anapata uhamisho.

Ya tano, Serikali kuhakikisha ina wanajeshi na polisi waliofundishwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu hasa wakati wa kuzima ghasia maana tumeshuhudia mara nyingi wanapoenda kuzima ghasia kazi yao wanajiingiza kazi ambazo ni chafu sana kama unajisi na uporaji wa mali wa wale ambao wangekuwa wanahitaji kuwalinda. Serikali iangalie itafanya namna gani kuhakikisha ina watu wa-forces ambao wana nidhamu ya hali ya juu.

Uchaguzi, ufanyike baada ya miaka mitano na Rais asipitishie vipindi viwili na awe chini ya sheria.

Pia ningependekeza mwananchi aruhusiwe kuandikisha ripoti au ku-report katika kituo chochote cha polisi anachotaka kuandikisha ripoti yake au ku-report jambo fulani na si lazima kwa kile kituo kiko karibu na yeye.

Pia ningependekeza Serikali yenye umoja wa kitaifa. Asanteni.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana mzee, tusonge mbele, wazee, tusonge mbele.

**David ole Simanga:** Kwa majina mimi naitwa David ole Simanga natoka sehemu ya Gwaso na yangu ni machache sana kwa maana tumesema mengi sana.

Ya kwanza ni, uhuru wa kuabudu na hiyo imetajwa sana na watu na tena naitilia mkazo ili tupate uhuru wa kuabudi katika Kenya.

Ya pili ni kuangalia maskini, hapa Kenya tunalia sana kwa sababu tunasema tumefilisika kiuchumi naomba Serikali kama inawezekana waangalie maskini wao. Kama inawezekana wawe wanalipa wale maskini kabisa angalau 5%.

Ya tatu ni kutoa mimba, hiyo nataka tutoe katika Kenya kabisa isiwe inakubalika kutoa mimba.

**Com. Githu Muigai:** Watoto wote wazaliwe.

**David ole Simanga:** Nimemaliza.

**Com. Githu Muigai:** Tunashukuru, wewe ni mzee unapenda watoto. Songa hapo Bwana. Jina lako?

**Moses Mbesa:** Kwa majina naitwa Moses Mbesa na natoka Ololwa Location na mimi ni candidate wa civic wa 2002. Ningelitaka kutaja jambo moja ama kupendekeza kuhusu maneno ya Majimbo. Mimi ninasikitika or I am rather disappointed kuona wananchi wakiongea maneno ya Majimbo. Ukiangalia yale mambo yanaendelea katika ulimwengu, ulimwengu unataka

unatangenezwa uiwe one global village na kama mnaona tume-revive East African Community, tuko na COMESA, iko European Union.

**Com. Githu Muigai:** Ikiwa wewe hutaki jimbo, pendekeza?

**Moses Mbesa:** Mimi napendekeza hivi, maneno ya Majimbo isahaulike maana wale watakoadhiriwa ni maskini. Mimi ukiniambia saa hii kwetu ni Mombasa nitaweza kuenda, ukimwambia maskini ataenda namna gani? Kwa hivyo tujaribu tusahau haya maneno tunasema ni ya Majimbo maana itawaadhiri maskini. Mkitengeneza hizo majimbo...*(incomplete)*.

Pili, ningetakaka kuongea kuhusu maneno ya worship, sisi tumekuwa na freedom of worship na sasa tunaona inianza kuwa abused. On a weekday like this wakati tuko kwa biashara kama hii ya leo ya Constitutional Review, unakuta mwingine ameweka speaker pale mwingine pale, unapigiwa na mtu simu hapa kwa soko hamwezi kuongea wana-worship, pale iko Kanisa nyingine. Tradition yetu katika Ngong tunajua tukiwa Bulbul tunajua Musikiti utalia saa ngapi na tumeji-tune tunajua hiyo itaongea. Siku hizi watu wana-interfere na hao Waislamu wakiomba, wanaweka loud speake. Hayai mambo yatafika point yatakuwa ni-explosive sana. Kwa hivyo kwanza hii ku-preach na ma-loudspeaker kwanza iangaliwe na wawe wana-preach katika specific places.

Ya tatu, kuhusu technical schools kweli ni lazima zirudishwe kwa maana zilikuwa zinasaidia sana mimi nikiwa mmoja wao, lakini zingetakiwa ziwe streamlined maana watu wengi wale walikuwa technical schools walienda in brain drain. Hakukuwa na bachelor of technology na vitu kama hivo, tulienda tu tukarudi kuwa tunaanza kusoma courses zingine tena.

Maneno vile vile ya elimu, wale watu wetu wote wanaenda kusomea ngambo lazima tujue vile watakavyo wakitusaidia sisi tukiwa kama wananchi, maana wakati wanaenda kusoma wanaenda kusoma na resources zetu. Wengine ni sisi tunawanfanyia mpaka ma-harambee wanaenda huko na wanapata kazi kubwa, kubwa na tungeliweza wawe mpaka tax yao inakatwa inaletwa humu nchini.

Jambo la mwisho ni kuhusu hii death penalty: Ni kweli mtu ikiwa anastahili kuuliwa maana amefanya makosa mabaya sana kama kuuwa ni sawa sawa lakini swali kubwa ni hili, wale wameuwa na hawajashikwa watafanywaje? Kwa hivyo ni vizuri tuondoe haya maneno ya death penalty maana hata wale wanauwa sio pengine ndio the main suspects, hata wale tuko na wao huku wengine ni wauwaji lakini wale hawajashikwa. Ni hayo tu, vile vile ningeshukuru Commissioners kwa kutusikiza na wakati ule mwingine mlikuja kukawa na vurugu mkaenda lakini tulikuwa na maoni na leo imekuwa siku mzuri sana.

**Com. Githu Muigai:** Tumerudi tena, asanteni.

**Kennedy:** Thank you Commissioners, my names are Kennedy Mudhanja and I have a few proposals which I would like to

make this evening.

1. Primary education; it is my proposal that primary education should be made free and compulsory to any school going child, and on that point I would request also and propose any child born of the a Kenyan parent whether locally or abroad should automatically gain Kenyan citizenship.
2. Healthcare: I am proposing that the Government should take care of our elderly, unapata wazee wameeka, hawana nguvu na hawana uwezo, pesa za hospitali hawana, pesa ya chakula hawana. I propose that the Government should set up some homes for the elderly and cater for their needs.
3. Political parties; majority of the political parties we have today are just mere tribal groupings, and it is my proposal that the Government should regulate them. Let us have 3 or four political parties which have a national outlook and can address issues, many of them are colourless and in pathetic situations.
4. Tribunals and Commissions of inquiry; funding these tribunals and these Commissions of inquiries takes up so much of public funds and they end up being thrown in the dust bin, we do not get to know the report or what came out of them. It is my proposal that these public hearings should be made public, I mean the Commissions and the tribunals should be made public like what happened to the Akiwumi Commission and some other hot issues. They should be made public so that the people can know what is going on.
5. Nominated Members of Parliament and Councillors, Parastatal Chiefs; it is my desire that these people should be vetted first by the Government before they are nominated. Before someone is taken as a CEO of any company, any Government entity, he should declare his wealth first and should go through scrutiny by the Parliament.
6. NSSF; at this point in time there is so much retrenchment going on and sackings. It is my desire and I strongly propose that the Government should come up with a set up such that once someone is sacked he should be given his dues immediately so that he can start something to develop himself rather than after sacking you may wait for 51 years or so. It is my desire that immediately one is sacked he should be given his dues. Thank you your Lordships for your time.

**Com. Githu Muigai:** Thank you very much na sasa mzee wa kutufungia kikao.

**Speaker:** Asante sana Commissioners, mambo mengi ambayo ningezungumza ama ningetoa points yametajwa, lakini kuna machache kama matatu ambayo nafikiri kama yamezungumzwa ama yametolewa proposals ningetaka kuongeza zaidi.

Moja ni irrigation, nchi yetu ya Kenya ni ya ukulima.

Pili ni traffic, hakuna aliye na gari anaweza kutoka hapa kuenda Mombasa na asipate askari barabarani. Njia zote kutoka Nairobi kuenda nje, Kisumu na kuenda pahali popote utakuta askari labda hamsini, na wote wanataka kitu. Wa kwanza alipokushika hakuna kitambulisho cha kuonyesha mwingine kwamba umeshakutana na askari mwingine.



Ya tatu ni cooperative movements, hizi ndizo nguvu za wananchi, wakichuna chochote kama kahawa ama nini itakuenda kumalizwa na watu watatu peke yake.

Kwa hivyo proposals zangu ni tatu na nikianza ya kwanza, traffic ingekuwa kutoka hapa iwe ni safari moja kama kutoka hapa naenda Mombasa, nikikutana na askari wa kwanza, wakiniandika anipatie charge nikielekea huko mbele wale wengine wote nitawaonyesha kwamba nimekutana na askari na nimekuwa charged kwa hivyo hakuna kitu cha kuzungumza zaidi hapo maana gari ni ile ile tu, sikubadilisha gari. Kwa hivyo kusimamishwa na mwingine anataka nimhonge.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumeelewa mzee.

**Speaker:** Kwa hivyo nikitoka hapa kuenda huko nikiwa-charged mwingine asinisimamishhe.

**Com. Githu Muigai:** Hiyo tumeelewa.

**Speaker:** Ya pili ni cooperative, wale wanachukua jukumu la kumaliza watu na njia moja. Ukitoka hapo kuenda hapo unaambiwa pesa zako zinachukuliwa na hakuna mahali pa kuwa accounted for kwa hivyo askari anachukua pesa na hakuna remarks. Tena inatakiwa turudishiwe na cooperative zile pesa ambazo tumetumia kwa hali ya uchumi kwa maana kutoka Kisumu kuja hapa ni pahali pazuri na maji ya Lake Victoria kuja hapa, hapa katika kuna mahali ambapo Wamaasai wangepata maji na wafanye irrigation bila charge. Badala yakutoa pipe kutoka Mombasa kupeleka Kisumu na hiyo maji haina gharama kubwa kama kukata mtaro kutoka Mombasa kuenda Kisumu. Kwa hivyo ninge-propose maji itoke Lake Victoria iingine laini hii tupate maji ya kutosha kufanya irrigation.

**Com. Githu Muigai:** Okay, hiyo tunashika vizuri wewe umesema Serikali ilete maji kama itatoa Loitoktok au Lake Victoria au popote lakini maji yafike hapa.

**Speaker:** Lakini kwanza maji ya hapo inakwenda nchi nyingine kama Lake Victoria, kwa hivyo tunataka maji kutoka Lake Victoria ije upande huu kila mtu apate maji ya kutosha. Asante sana.

**Com. Githu Muigai:** Asante sana. Sasa tumefika mwisho wa kikao chetu cha leo.

**(Interjection)**

**Samuel Kinyanjui:** .....(Inaudible)

**Com. Githu Muigai:** Okay, hakuna mtu ataenda nyumbani bila kusema. Chukua dakika mbili.

